CHUO CHA USTAWI WA JAMII

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO



# JARIDA LA MTANDAONI

JANUARI - MACHI, 2026



Pichani ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Aliyevaa nguo nyekundu) kulia kwake ni Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Dkt. Joyce Nyoni. Kushoto kwake ni Mratibu wa Kituo cha Huduma za kisaikolojia Bi Rufina Khumbe akifuatiwa na Mbunge wa Kinondoni Abbas Tarimba pamoja na Naibu Mkuu wa Taasisi Fedha na Mipango Dkt. Zena Mabeyo

## ZIARA YA MH. MARYPRISCA MAHUNDI CHUO CHA USTAWI WA JAMII SERIKALI KUENDELEA KUIMARISHA CHUO CHA USTAWI WA JAMII, KUTOA WATAALAMU BORA

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema itaendelea kukiimarisha Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kwa ajili ya kuendelea kuzalisha wataalam wenue uwezo wa kukabiliana na changamoto za kijamii na kuchangia maendeleo ya taifa, sambamba na kuboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa ziara yake Februari 23, 2026 katika Chuo hicho mkoani Dar Es Salaam, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi amesema Serikali inatambua nafasi ya chuo hicho katika kuandaa wataalamu wa ustawi wa jamii watakaosaidia kuimarisha huduma za kijamii nchini.

Amesema Serikali itaendelea kushirikiana na uongozi wa chuo hicho pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha changamoto za miundombinu ikiwemo upungufu wa hosteli na kumbi za mihadhara zinapatiwa ufumbuzi ili kuboresha zaidi mazingira ya kujifunza.

“Serikali inatambua kuwa uwekezaji katika miundombinu ya Chuo cha Ustawi wa Jamii ni uwekezaji katika ustawi wa taifa, hatuwezi kuzungumzia maendeleo jumuishi bila kuwa na taasisi imara zinazozalisha wataalamu wa kusimamia ustawi wa jamii, afya ya akili, malezi, ujumuishi na haki za makundi maalum,”

Amesema Serikali itaendelea kushirikiana na uongozi wa chuo hicho pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha changamoto za miundombinu ikiwemo upungufu wa hosteli na kumbi za mihadhara zinapatiwa ufumbuzi ili kuboresha zaidi mazingira ya kujifunza.

amesema na kuongeza:"Tutahakikisha ujenzi wa miundombinu ya chuo hiki ni moja ya vipaumbele vya serikali, lengo ni kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi kuhakikisha miradi ya ujenzi inatekelezwa kwa wakati na kuongeza ubora wa mazingira ya kujifunzia.”

Amesema kwa mwaka wa masomo 2025/2026 chuo hicho kina jumla ya wanafunzi 5,868 ambapo wanawake ni 3,823 na wanaume 2,045, hali inayoonesha ongezeko la udahili na uhitaji mkubwa wa wataalamu wa ustawi wa jamii nchini.



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akipanda mti ndani ya Chuo cha Ustawi wa Jamii Kampasi ya Dar es Salaam

## ZOEZI LA UPANDAJI MITI KUMBUKIZI YA KUZALIWA MH. RAIS SAMIA

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Chuo Cha Ustawi wa Jamii, Dkt. Joyce Nyoni ameongoza baadhi ya wajumbe wa Menejimenti pamoja na rais wa Serikali ya Wanafunzi (ISWOSO) katika zoezi la kupanda miti ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunza mazingira katika kuadhimisha kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa Januari 27, 2026.

Katika upandaji huo menejimenti, watumishi na wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wametuma salamu za kumtakia heri: “Tunamtakia Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan afya njema, maisha marefu, na kila la kheri katika majukumu yake ya kila siku ya kuongoza Taifa letu la Tanzania.”



rais wa Serikali ya Wanafunzi Bw. Abdallah Zidane akipanda mti ndani ya Chuo cha Ustawi wa Jamii Kampasi ya Dar es Salaam



Pichani ni Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni (aliyekaa Katikati) akiwa pamoja na Waratibu wa Mradi na Waelimisha Rika wapya kutoka Kampasi ya Dar es Salaam

## MAFUNZO YA WAELIMISHA RIKA WAPYA

Na Mwandishi Wetu

WAELIMISHAJI rika wapya 15 kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) waliochaguliwa hivi karibuni wamepatiwa mafunzo ya ujuzi wa vitendo na msingi wa maadili yanayohitajika chini ya mradi wa UNESCO.

Lengo ni kusaidia na kuongoza kwa ufanisi wanafunzi wenzao, ikiwa ni hatua muhimu kuelekea utetezi unaoongozwa na vijana na kupanua usaidizi wa kina kuhusu afya na haki za jinsia na uzazi ndani ya kampasi.

"Kwa siku tatu zenye matokeo, wawezeshaji wataalam waliwaongoza washiriki kupitia moduli muhimu za Ujana na Ujinsia UKIMWI, VVU na magonjwa ya zinaa, mahusiano yenye afya, ukatili wa kijinsia (GBV), na usimamizi wa rasilimali,"amesema Mratibu wa Programu ya Waelimisha rika, Rufina Khumbe.

Amesema mafunzo hayo yameibua ushiriki na ushirikishwaji wa kina yakitoa nafasi kwa mazungumzo ya wazi yaliyojikita kwenye kwenye ukweli, heshima na tafakari.

Waelimisha rika walionyesha ari na kujitolea kwa hali ya juu, tayari kutumikia jumuiya ya wanafunzi wenzao wa Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa ujasiri, huruma, na weledi katika safari yao yote ya utekelezaji wa mradi wa O3+.

Wakiwa wamewezeshwa na maarifa, vijana hawatengenezi maisha yao ya baadaye tu bali wanaunda mustakabali wa jamii zao.




Pichani ni Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akiwasilisha mada katika Kongamano la Wanawake lililofanyika Dar es Salaam

## DKT. JOYCE: FAMILIA IMARA MSINGI WA TAIFA LENYE WATU WENYE USTAWI

MKUU wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dkt. Joyce Nyoni amesema familia ni taasisi ya kwanza ya kijamii ambayo binadamu huikuta kabla ya shule, kanisa au msikiti na ajira.

Aidha, amesema ndani ya familia ndipo mtoto hujifunza lugha, maadili, heshima pamoja na kujifunza namna ya kuishi na wengine.

"Tunaposema familia yangu, Taifa langu" tunamaanisha kuwa ubora wa Taifa ni kioo cha ubora wa familia zake,"amesisitiza.

Dkt. Joyce ameyasema hayo leo Machi 6,2026 wakati akiwasilisha mada kuhusu familia yangu Taifa langu katika Kongamano la Wanawake 2026 lililoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani katika Ukumbi wa Mkataba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wanawake na Makundi Maalum, Mh. Dkt.Dorothy Gwajima, amesema:

"Ikiwa familia zetu zina amani, Taifa litakuwa na amani Ikiwa familia zetu zina misingi ya haki, Taifa litakuwa na misingi ya haki,ikiwa familia zetu zina usawa, Taifa litakuwa jumuishi."

Aidha,amesema kuwa amani ya Taifa huanzia kwenye amani ya familia na kwamba familia yenye migogoro, dhuluma na ukatili huathiri afya ya akili ya watoto.

"Watoto wanaokulia katika mazingira ya vurugu wana uwezekano mkubwa wa kuendeleza vurugu, kukosa utulivu wa kisaikolojia, kushindwa kufikia uwezo wao wa juu,"amesema Dkt. Gwajima ambaye kitaalum ni Daktari wa Sosholojia.



Mtumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Fidea Nyenga akitoa elimu juu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Mailisita

## WANAWAKE ISW KAMPASI YA KISANGARA WATOA MSAADA KITUO CHA AFYA KIJITONYAMA, DAR

MAADHIMISHO ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani Mkoa wa Kilimanjaro yaliyofanyika Machi 9,2026 katika Wilaya ya Hai, katika viwanja vya Shule ya Sekondari Mailisita.

Mgeni rasmi katika maadhimisho haya alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mh. Nurdin Babu.

Katika maadhimisho hayo zilifanyika shughuli mbalimbali za kijamii na kielimu, ambapo Machi 5, mwaka huu, watumishi wanawake wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara walipata nafasi ya kutoa elimu ya kujitambua, kujiamini na hedhi salama kwa mabinti wa Shule ya Sekondari Kisangara iliyopo Wilayani Mwanga.



Watumishi wanawake wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Katika picha ya pamoja wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani

Mafunzo hayo yaliambatana na ugawaji wa taulo za kike (pads) kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo katika kipindi cha hedhi wakiwa shuleni.

"Machi 06, 2026 tuliungana na wanawake wa tuliungana na wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake kiwilaya yaliyofanyika Tarafa ya Usangi. Katika maadhimisho hayo tulipata fursa ya kutoa elimu kuhusu programu zetu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto pamoja na Ustawi wa Jamii zinazotolewa katika chuo chetu,"amesema.

Aidha, amesema sambamba na hilo, wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga walitoa msaada wa mahitaji muhimu kwa watoto wenye mahitaji maalum, ikiwa ni pamoja na taulo za kike (pads), pampas, mabegi ya shule na mahitaji mengine muhimu ili kusaidia ustawi na maendeleo yao.

"Kwa pamoja tunaendelea kuunga mkono jitihada za kuwawezesha wanawake na watoto wa kike, kuimarisha elimu, afya na ustawi wao katika jamii,''amesema.



Pichani ni Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mailisita iliyopo mkoani Kilimanjaro wilaya ya Hai



Pichani ni Afisa Kazi Mwandamizi Neema Daniel Msyaliha katika uzinduzi wa Baraza jipya la Wafanyakazi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii

## BARAZA JIPYA LA WAFANYAKAZI USTAWI WA JAMII LAZINDULIWA

AFISA Kazi Mwandamizi Neema Daniel Msyaliha kutoka Idara ya kazi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano Machi 23, 2026 kwa niaba ya Kamishna wa kazi, amezindua Baraza jipya la Wafanyakazi la Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambalo litahudumu kwa miaka mitatu.
Katika kikao hicho, Baraza la Wafanyakazi lilipokea na liliwatambua na kuwathibitisha wajumbe wapya kutoka katika idara na vitengo mbali mbali.

Katika hatua nyingine baraza lilifanya uchaguzi wa katibu na Katibu Msaidizi wa baraza hilo jipya na baadaye kujadili masuala mbali mbali ya maendeleo ya taasisi ikiwepo Dira ya mpango mkakati wa Taasisi pamoja na Kupitia Rasimu ya Bajeti ya Taasisi ya Mwaka 2026/2027.



Pichani ni Wafanyakazi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii waliohudhuria uzinduzi wa Baraza jipya la Wafanyakazi

## KITUO CHA UBUNIFU CHAENDESHA MAFUNZO YA FIKRA BUNIFU

CHUO cha Ustawi wa Jamii, kupitia Kituo cha Ubunifu (Digital Innovation Center), Machi 27, 2026 kimeendesha Warsha ya Design Thinking na Pitching, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mashindano ya Ubunifu wa Kidijitali 2026.

Warsha hiyo iliwakutanisha wanafunzi wabunifu na kuwapatia mafunzo ya kina kuhusu utambuzi wa changamoto, ubunifu unaomlenga mtumiaji (user-centered design), pamoja na mbinu bora za uwasilishaji wa mawazo (pitching).

Aidha, washiriki walipata fursa ya kuboresha mawazo yao na kujiimarisha katika kubuni suluhisho zenye tija na zinazoweza kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Chuo kinaendelea kujikita katika kukuza ubunifu, fikra bunifu, na ujuzi wa vitendo kwa wanafunzi, sambamba na vipaumbele vya taifa katika kuwawezesha vijana na kukuza matumizi ya teknolojia katika maendeleo.



Pichani ni wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii waliohudhuria Warsha iliyoandaliwa na Kituo cha Ubunifu



Prof. Sotco Komba
Naibu Mkuu wa Taasisi (Taaluma, Utafiti, na Ushauri Elekezi)



Dkt. Zena Mabeyo
Naibu Mkuu wa Taasisi (Mipango, Fedha na Utawala)

Viongozi wawili wa Menejimenti ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii viongozi wamepata teuzi kama ifuatavyo.

Dkt. Zena Mnasi Mabeyo aliteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Taasisi (Mipango,Fedha na Utawala) kwa kipindi cha miaka minne (04) uteuzi ambao umeanza Desemba 01, 2025.

Naye, Prof. Sotco C. Komba pia aliteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Taasisi (Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi) kwa kipindi cha miaka minne kuanzia Februari 2026.




## CHUO CHA USTAWI WA JAMII NA KONGAMANO LA KIMATAIFA

**Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kinaandaa Kongamano la Kimataifa linaloitwa "Kuwezesha Watu na Kubadilisha Jamii: Njia za Ustawi Endelevu"**

**Kongamano hili linatarajiwa kufanyika Juni 5, 2026 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam, kwa lengo la kutoa fursa ya kipekee kwa wanazuoni, watafiti, watunga sera, na wadau kubadilishana mawazo, ujuzi, na uzoefu wa mbinu shirikishi na bunifu za kuboresha ustawi wa jamii na maendeleo ya binadamu kwa ujumla.**

**Katika Mkutano huo, wadau wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii kutoka nchi zaidi ya kumi na moja duniani watatoa mada mbalimbali katika nyanja za Ushiriki wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake; Maendeleo, Ulinzi na Haki za Mtoto; Ujasiriamali, Ubunifu na Mabadiliko ya Kidijitali; Afya ya Akili na Ustawi wa Jamii; Elimu ya Fedha na Maendeleo ya Biashara; na Uwezeshaji Mahali pa Kazi.**



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya jamii wakiwasilishiwa taarifa ya maendeleo ya mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII YATEMBELEA KAMPASI ZA ISW

**KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ikiwasili Machi 17, 2026 kukagua mradi wa ukumbi wa mihadhara unaojengwa katika kampasi ya Dar es Salaam.**

**Kamati hiyo iliyoongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo Dkt. Regina Malima ilipokelewa na Mh. Naibu Waziri Mhandisi MaryPrisca Mahundi pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dkt. John Jingu wakiwa na Menejimenti ya Chuo cha Ustawi wa Jamii.**



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya jamii wakikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara

**Aidha, wamepomgeza baada ya kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa na Chuo cha Ustawi wa Jamii, lakini pamoja na jinsi kampasi hiyo inavyoandaa walezi na wakufunzi wa kozi ya makuzi, malezi na maendeleo ya awali ya watoto wakionyeshwa darasa mfano ambalo linatoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi hao.**

**"Binti kama huyu akimaliza haya mafunzo hapa, akapewa mtaji wa kwenda kianzisha kituo chake cha kuelea watoto mchana atakuwa amefanikiwa kimaisha na pia ameongeza utatuzi wa malezi ya watoto katika jamii yetu'' amesema Dkt. Regina Malima.**

# KURASA RASMI ZA CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**INSTAGRAM**
ISW_OFFICIAL_TZ

**TWITTER (X)**
TAASISIYAUSTAWI

**WHATSAPP CHANNEL**
CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**YOUTUBE CHANNEL**
CHUOCHAUSTAWIWAJAMII

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

210 Shekilango Road
P.O. BOX 3375
14113 Kijitonyama
Dar es Salaam
+255735509090
+255677111200
+255716121096
or
info@isw.ac.tz